

Shairi hili la Mwandani liliandikwa na Bi Salma Juma wa Zanzibar, ambaye anazungumzia Mapenzi ya kweli. Ameliandika shairi hili kwa ajili ya mwandani wake. Hili Shairi linazungumzia mapenzi ya kweli ambayo baadhi yetu tunayachukulia juu juu tu. Hivyo Bi Salma anatumkumbusha tena, umuhimu wa mapenzi ya kweli.

## MWANDANI

1. Hadhira ninaijuza, kwa yote niliyofunzwa.  
Mapenzi niloyakuza, mwandani kumliwaza.  
Ni pekee nayatunza, yako nimeyatukuza.
2. Yangu ya ndani fuadi, naahidi takuenzi.  
Mapenzi yaloshtadi, si kwa sababu simanzi.  
Lisania meshadidi, nyamae nzuri azizi.
3. Mwandani ulo wa ndani, wangu ninakutamani.  
Baidi yako hanini, nakupenda niamini.  
Si yeyote insani, aliyekuzidi mwandani.
4. Mapenzi yako mwandani, yanaishinda asali.  
Mapenzi yenye imani, thabit tena ya kweli.  
Mpenzi nakutamani, kwa yeyote ile hali.
5. Nashindwa kujitambua, Nashindwa kuvumilia.  
Natafuta kila njia, Ridhaa kuifikia.  
Tafrani nimekuwa, azizi nakuhitajia.
6. Natamani ya mwandani, Naumia kwa mwandani.  
Ungefungua moyoni, ukaona tathmini.  
Kwa ninavyokuthamini, Nakutamani mwandani.
7. Mwandani usinikhini, nakuomba niamini.  
Umuamini Manani, Nakulia na yamini.  
Ni kubwa yako thamani, hakika nakuthamini.  
  
Pokea hii zawadi.  
Wengi hawaifaidi.  
Nyoyo zao hufisidi.  
Na chuki zao huzidi.

Waitafuta kwa dhati Na kwa miguu ya futi.  
lakini hawaipati.

**SALMA JUMA**  
**Zanzibar-Tanzania**